



Dodoma Head Office P.O.Box 453 Dodoma, Tanzania. Tel +255 026 2323456/7

**TAARIFA KWA UMMA
MAJARIBIO YA MFUMO WA MANUNUZI YA UMEME WA MALIPO KABLA YA MATUMIZI
(LUKU) KATIKA KITUO CHA KUJIKINGA NA MAJANGA**

JUNI 6, 2022.

Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) linawataarifu wateja wake kuhusu maboresho ya mfumo wa manunuzi ya umeme kwa wateja wanaolipia kabla ya matumizi (LUKU) kupitia mifumo iliyopo katika kituo cha kujikinga na majanga (Disaster Recovery).

Zoezi la maboresho hayo linatarajiwa kufanyika muda wa saa sita usiku Alhamisi ya tarehe 09 Juni, 2022. Wakati wa zoezi hili wateja wa LUKU watakosa huduma ya malipo kwa muda wa masaa mawili yaani saa 6 mpaka saa 8 usiku.

Kutokana na zoezi hilo Shirika linashauri wateja wake kununua umeme wa ziada ili kuepuka usumbufu unaoweza kujitokeza iwapo zoezi litachukua muda zaidi kwa sababu zitakazokua nje ya uwezo wa wataalamu wetu.

Maboresho haya muhimu yanalenga kuongeza ufanisi kwenye mfumo wa manunuzi ya umeme ili kuwahudumia wateja wetu ipasavyo pale inapotokea hitilafu ya aina yoyote katika kituo chetu kikuu cha mifumo.

Shirika linaomba radhi kwa usumbufu wowote utakaojitokeza.

Imetolewa Na;
OFISI YA UHUSIANO,
TANESCO- MAKAO MAKUU,
DODOMA.